KARATASI RASMI YA UCHAGUZI
UCHAGUZI WA KILA MWAKA WA MJI
BURLINGTON, VERMONT
TAREHE 1 MACHI, 2022
KATA YA 4

MAAGIZO KWA WAPIGAJI KURA

1. Tumia PENSELI au KALAMU NYEUSI kujaza mduara. ⬬
2. Ili kumpigia kura mtu ambaye jina lake limechapishwa kwenye karatasi ya uchaguzi, jaza mduara ulio upande wa kulia wa jina la mtu huyo.
3. Ili kumpigia kura mtu ambaye jina lake halijachapishwa kwenye karatasi ya uchaguzi, andika au uambatishe jina la mtu huyo kwenye nafasi iliyopo na ujaze kwenye mduara upande wa kulia wa mstari wa kuandika. ⬬
4. Usiwapigie kura wagombea zaidi ya waliolezwa katika “usipige kura kumchagua zaidi ya mgombeaji #” aongoze ofisi fulani.
5. Ukifanya makosa, rarua au uiharibu karatasi ya uchaguzi, kisha uirudishe kwa afisa wa uchaguzi na upewe karatasi nyingine. USIIFUTE.

KWA DIWANI WA MJI

Kipindi cha Miaka Miwili
Usipige kura kumchagua zaidi ya mgombeaji MMOJA

SARAH CARPENTER ◯
Burlington DEMOCRATIC

◯

(Andika ndani)

KWA KAMISHNA WA SHULE

Kipindi cha Miaka Miwili
Usipige kura kumchagua zaidi ya mgombeaji MMOJA

MARTINE LAROCQUE GULICK ◯
Burlington

ERICKA BUNDY REDIC ◯
Burlington

◯

(Andika ndani)

KWA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

Kipindi cha Miaka Mitatu
Usipige kura kumchagua zaidi ya mgombeaji MMOJA

LINDA BELISLE ◯
Burlington INDEPENDENT

◯

(Andika ndani)

TIA ALAMA KWENYE PANDE ZOTE MBILI ZA KARATASI YA UCHAGUZI

SAMPLE

MASWALI

MAAGIZO KWA WAPIGAJI KURA

1. ILI UPIGE KURA KUCHAGUA lolote kati ya maswali yafuatayo, jaza mduara ulioandikwa NDIYO.
2. ILI UPIGE KURA KUTOCHAGUA lolote kati ya maswali yafuatayo, jaza mduara ulioandikwa HAPANA.
3. ILI KUPIGA KURA, JAZA MDUARA NAMNA HII: ⬬
4. Ukifanya makosa, rarua au uiharibu karatasi ya uchaguzi, kisha uirudishe kwa afisa wa uchaguzi na upewe karatasi nyingine. USIIFUTE.

1. UIDHINISHAJI WA BAJETI YA SHULE YA MWAKA WA KIFEDHA WA 2023

"Je, wapiga kura wa wilaya ya shule wanaipa idhini bodi ya shule kutumia $98,232,381 ambayo ni kiasi ambacho bodi ya shule imebaini kinahitajika kwa mwaka wa kifedha unaofuata?

Inakadiriwa kuwa bajeti hii inayopendekezwa, ikiidhinishwa, itasababisha matumizi ya elimu ya $19,310.56 kwa kila mwanafunzi aliyepewa nafasi sawa. Matumizi haya yaliyokadiriwa kwa kila mwanafunzi aliyepewa nafasi sawa ni ongezeko la 13.13% zaidi ya matumizi ya mwaka huu. Matumizi kwenye kiwango hiki yanaweza kuchangia upunguaji wa kiwango cha kodi ya mali wa 6.98% (kadirio la sasa)."

NDIYO ⬭
HAPANA ⬭

2. ONGEZEKO LINALOPENDEKEZWA KWENYE KIWANGO CHA JUMLA CHA KODI YA MFUKO

"Je, kiwango cha jumla cha juu cha kodi ya jiji kulingana na Sehemu ya 99 ya City Charter kinaweza kuongezwa kwa $0.04 kutoka $0.1952 hadi $0.2352, ongezeko la 5.5% kwenye kiwango cha jumla cha kodi ya jiji cha FY23?"

NDIYO ⬭
HAPANA ⬭

3. UIDHINISHAJI WA KUTOA DHAMANA ZA MANISPAA KWA AJILI YA MIRADI MIKUU

"Je, Baraza la Jiji litaidhinishwa kutoa dhamana za manispaa au noti katika mfululizo mmoja au zaidi kwa kiwango kisichozidi Dola Milioni Ishirini na Tatu na Laki Nane ($23,800,000) kwa madhumuni ya kufanikisha mfululizo wa miradi mikuu ya maboresho, ubadilishaji na ukarabati ndani ya Jiji, ikiwa ni pamoja na lakini si tu ubadilishaji wa malori ya kukabiliana na moto na mifumo ya mawasiliano ya dharura, kukarabati vituo kumi vinavyomilikiwa na jiji na njia za wanaotembea kwa miguu za jiji za maili kumi na utengaji wa fedha za ruzuku za serikali za mitaa kwa miradi mikuu inayoendelea au inayokuja iliyokusudiwa kudumisha majengo na huduma za Jiji, kuepuka gharama zaidi za matengenezo na ukarabati na kuendeleza miradi ya kuboresha Jiji na miundomsingi yake kwa sharti kwamba Jiji likifaulu kupata fedha nyingi zaidi ya mipango ya sasa, zinazoweza kutumiwa badala ya Dhamana za Manispaa, Utawala utaipa kipaumbele akiba ya walipa kodi kuwa lengo kwa sharti jingine linalosema kuwa huenda lisitenge tena mapato ya dhamana kwa uwekezaji mwingine, isipokuwa kwa idhini bayana ya Baraza la Jiji kuhusu utengaji fedha?"

NDIYO ⬭
HAPANA ⬭

4. KUAHIDI MKOPO WA JIJI ILI KULINDA DENI KWA AJILI YA MABORESHO YA UMMA NDANI YA DOWNTOWN TIF DISTRICT

"Je, baraza la Jiji litaidhinishwa kuahidi imani kamili na mkopo wa Jiji ili kulinda deni au kufanya malipo ya moja kwa moja kwa madhumuni ya kufadhili boresho moja au maboresho zaidi ya umma na gharama zinazohusika ambazo zinatokana na miradi inayosaidia Downtown Tax Increment Financing (TIF) District, haswa:

(a) **Usitawishaji wa Main Street Streetscape:** Kwa bloku sita kati ya South Union Street na Battery Street ikiwa ni pamoja na mikingamo yote: kujumuisha usitawishaji wa barabara ya mjini, maji ya mvua, huduma msingi za umma, taa, usafiri na kujumuisha uhamishaji au usitawishaji wa sehemu inayoitwa "mfereji wa maji machafu ya korongo" kutoka mahali ilipo saa kuvuka bloku ya kati kutoka College Street hadi Main Street katika bloku kati ya South Union na South Winooski Avenue;

(b) **Gharama Husika:** malipo au fidia ya gharama husika zinazostahiki za TIF ambazo Jiji lilipata kwa ajili ya uundaji, utekelezaji na usimamizi wa Downtown TIF District, ikiwemo gharama zilizolipwa wachuuzi, washauri wa nje na ada mbalimbali husika na matumizi mengine yanayohusiana na wilaya ya TIF na pia matumizi ya moja kwa moja ya manispaa kama vile gharama za idara au wafanyakazi zinazohusiana na kuunda au kusimamia wilaya hadi kufikia pale wanalipwa kutoka kwenye ongezeko la ushuru wa manispaa na si wa elimu na vinginevyo wanafidiwa kwa mujibu wa sheria;

kwa kiasi cha mtaji kutozidi $25,920,000 (kitakachofanya jumla ya deni la Downtown TIF District lililoidhinishwa tangu uundaji wa Downtown TIF District kuwa $35,920,000, ambapo $10,000,000 ziliidhinishwa awali na wapiga kura na $5,420,000 zilikopwa awali kwa $4,580,000 zilizoidhinishwa lakini bado hazijakopwa) na kutoa dhamana, noti au kutoa mikopo ya fedha ndani ya shirika kwa madhumuni hayo na kutumia hadi $1,470,000 za gharama husika, zitakazofanya gharama za jumla husika zilizoidhinishwa na wapiga kura kuwa $1,848,000 kwa kuelewa kwamba ongezeko la ushuru kutoka kwenye majengo yaliyo ndani ya Downtown TIF District litaahidiwa na kutengwa kwa ajiili ya deni kama hilo au gharama za moja kwa moja za maboresho; na kuelewa zaidi kwamba Jiji linaweza kutumia zaidi ya hitaji la chini sana la sheria iliyowekwa ya 75% ya ongezeko lote la manispaa, hadi na ikiwemo 100% ya kiwango sawa, ili kutimiza majukumu ya kifedha ya Downtown TIF District?"

NDIYO ⬭
HAPANA ⬭

5. MABADILIKO YA MKATABA YANAYOPENDEKEZWA KUONDOA MAMLAKA YA BARAZA LA JIJI KUDHIBITI WAFANYABIASHARA WA NGONO

"Je, Mkataba wa Jiji la Burlington, Sheria za 1949, Namb. 298 kama zilivyorekebishwa, kurekebishwa zaidi kwa kuondoa kabisa §48(7) ili kuondoa kwenye mamlaka yaliyotajwa ya Baraza la Jiji uwezo wa:

~~(7) Kuzuia na kukomesha nyumba za mwenendo mbaya na kuwaadhibu makahaba sugu na watu wanaondamana nao."~~

NDIYO ⬭
HAPANA ⬭

TIA ALAMA KWENYE PANDE ZOTE MBILI ZA KARATASI YA UCHAGUZI

SAMPLE